



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TANGAZO LA MWALIKO KWA TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZENYE NIA  
YA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA  
MADIWANI KATIKA KATA 23 ZA TANZANIA BARA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha uchaguzi mdogo wa Madiwani katika kata 23 za Tanzania Bara. Uchaguzi huo utafanyika siku ya jumatano tarehe 20 Machi, 2024 katika kata zifuatazo: -

Na.	Mkoa	Halmashauri ya	Kata
1.	Dar es Salaam	Manispaa ya Kigamboni	Kimbiji
2.	Kigoma	Manispaa ya Kigoma/Ujiji	Kasingirima
3.	Tabora	Manispaa ya Tabora	Ndevelwa
4.	Pwani	Mji Kibaha	Msangani
		Wilaya ya Bagamoyo	Fukayosi
		Wilaya ya Kibiti	Mlanzi
5.	Ruvuma	Mji Mbinga	Utiri
		Wilaya ya Songea	Mbingamhalule
6.	Geita	Wilaya ya Mbogwe	Isebya
7.	Lindi	Wilaya ya Kilwa	Kibata
8.	Mara	Wilaya ya Musoma	Mshikamano
		Wilaya ya Butiama	Busegwe
9.	Mbeya	Wilaya ya Kyela	Nkokwa
10.	Morogoro	Wilaya ya Mlimba	Kamwene

Na.	Mkoa	Halmashauri ya	Kata
11.	Mtwara	Wilaya ya Nanyumbu	Chipuputa
12.	Mwanza	Wilaya ya Sengerema	Buzilasoga
		Wilaya ya Kwimba	Mhande
13.	Rukwa	Wilaya ya Nkasi	Kabwe
14.	Simiyu	Wilaya ya Meatu	Bukundi
15.	Tanga	Wilaya ya Muheza	Mkuzi
		Wilaya ya Mkinga	Boma
			Mtimbwani
			Mayomboni

Kwa mujibu wa kanuni ya 3 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Tume ina wajibu wa kutoa elimu ya mpiga kura nchi nzima, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka taasisi na asasi za kiraia nchini zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura katika uchaguzi mdogo wa madiwani katika kata 23 za Tanzania Bara kama ilivyoainishwa kwenye jedwali.

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura zinatakiwa kuwasilisha maombi yao kwa njia ya barua pepe: [info@nec.go.tz](mailto:info@nec.go.tz) au [uchaguzi@nec.go.tz](mailto:uchaguzi@nec.go.tz) Maombi hayo yatapokelewa kuanzia tarehe 15 hadi tarehe 20 Februari, 2024.

Barua ya maombi inatakiwa kuainisha mambo yafuatayo kuhusu taasisi au asasi husika: -

- i. Iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;
- ii. Iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;
- iii. Ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu, wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa wanapaswa wawe Watanzania;


- iv. Katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;
- v. Iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na
- vi. Iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

Aidha, maombi hayo yanatakiwa kuambathishwa na: -

- i. Nakala au kivuli cha cheti cha usajili;
- ii. Nakala au kivuli cha Katiba ya taasisi au asasi ya kiraia;
- iii. Majina matatu ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi ya kiraia;
- iv. Anuani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake; na
- v. Ratiba itakayoonesha tarehe na mahali elimu ya mpiga kura itakapotolewa katika halmashauri husika.

Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa taasisi au asasi za kiraia zitakazopewa kibali.

Limetolewa leo tarehe 15 Februari, 2024 na:



Kailima, R. K

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**